



Rais wa watu?

Tathmini na matarajio ya wananchi kwa serikali ya awamu ya tano

1. Utangulizi

Baada ya uchaguzi mkuu mwezi Oktoba mwaka 2015, serikali, chini ya uongozi wa Rais John Pombe Magufuli, imejikita katika kufanya mabadiliko kwa kasi kubwa sana. Mapambano yake dhidi ya vitendo vya rushwa na ukwepaji wa kodi bandarini, kufuta ada za shule, kuwaondoa hadharani watumishi wa umma wanaotuhumiwa kufanya vitendo viovu pamoja na kuzuia uingizwaji wa sukari nchini, ni mionganini mwa masuala yaliowavutia vyombo vya habari na wananchi kwa ujumla. Msemo wa "hapa kazi tu" na "tumbua majipu" yamegusa hizia za wananchi wengi.

Wakati huo huo, serikali imekuwa ikikosolewa kutoka maeneo mbalimbali. Je, hatua stahiki zinafuatwa wakati wa kuwaondoa watumishi wa umma? Je, vitendo vya kuzuia shughuli za vyama vya siasa na kusitisha matangazo ya moja kwa moja ya bunge ni vya kidemokrasia au vya "kidikteta"? Na je, jitihada kali za ukusanyaji wa kodi zimeathiri sekta binafsi? Muhtasari huu unabainisha maoni ya wananchi katika miezi ya awali ya uongozi wa Rais Magufuli.

Je, ni vitendo gani vya Rais ambavyo vimejipatia umaarufu mkubwa? Wananchi wanaonaje kampeni ya 'tumbua majipu' ya kuwaumbua watumishi wa umma wabadhilifu hadharani? Je, wananchi wanaona mabadiliko yoyote kwenye utendaji wa serikali? Takwimu za muhtasari huu zinatokana na utafiti wa *Sauti za Wananchi* unaofanywa na taasisi ya Twaweza. *Sauti za Wananchi* ni utafiti wenye uwakilishi wa kitaifa unaotumia simu za mikononi. Taarifa kwa ujumla kuhusu mbinu za utafiti huu zinapatikana kuititia

www.twaweza.org/sauti. Takwimu za muhtasari huu zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,813 kutoka kundi huru la pili la Sauti za Wananchi. Hii ikiwa ni awamu ya kumi na moja ya simu zilizopigwa kwenye kundi jipya, kati ya tarehe 4 Juni na tarehe 20 Juni, mwaka 2016. Utafiti huu una uwakilishi wa Tanzania bara pekee.

Sauti za Wananchi imepata aina mbili tofauti za takwimu: takwimu za maoni – maoni ya wananchi kwenye masuala mbalimbali; na ufuataliji wa takwimu – taarifa za wananchi zinatokana na uzoefu wao kwenye huduma za umma zitolewazo na serikali. Muhtasari huu kwa kiwango kikubwa umebeba takwimu, zinazoakisi mitazamo na maoni ya wananchi.

Matokeo muhimu ni:

- Mwananchi mmoja kati ya ishirini anapata taarifa za kutosha kuhusu masuala ya siasa nchini.
- Vitendo maarufu vya Rais Magufuli ni pamoja na kuwafuta wafanyakazi hewa, elimu ya msingi bure, na kuwasimamisha kazi watumishi wa umma wabahirifu, maarufu kama 'kutumbua majipu'.
- Kitendo cha Rais Magufuli ambacho hakijapata umaarufu sana ni kuzuia uingizaji wa sukari nchini na kutoa bei elekezi ya sukari.
- 96% ya Watanzania wapongeza utendaji wa Rais Magufuli tangu alipoingia madarakani.
- 68% ya Watanzania wapongeza utendaji wa wabunge wao.
- Wananchi watatu kati ya wanne wanasema watendaji waondolewe pale tu kunapokuwa na udhibitisho wa kufanya vitendo viovu.

2. Mambo kumi kuhusu maoni ya wananchi juu ya utendaji wa serikali mpya

Jambo la 1: Wananchi wanawafahamu wawakilishi wao


Zaidi ya wananchi tisa kati ya kumi wanawafahamu madiwani wao (92%), wabunge wao (92%) na Rais wao (98%). Pia, idadi kubwa (96%) inamfahamu Afisa Mtendaji wa Kijiji, na asilimia 79% ya wananchi wanamfahamu Afisa Mtendaji wa Kata. Wananchi wachache wanamfahamu voingozi wa kuteuliwa: Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya (21%), Mkuu wa Wilaya (40%) na Mkuu wa mkoa (38%).

Wananchi wana uzoefu wa kukutana na watendaji wa ngazi za chini kama vile Afisa Mtendaji wa Kijiji (47%), Diwani (41%) na Afisa Mtendaji wa Kata (31%). Lakini wananchi wachache wamekutana na mbunge (25%), Mkuu wa Wilaya (11%), Mkuu wa Mkoa (5%) na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya (4%).

Idadi hii inafanana kutoka kwenye makundi mbalimbali kiumri, kijinsia na maeneo ya mjini/vijiji. Watu wazima na wanaume huwafahamu na wamekutana na viongozi walijotajwa, huku wale wanaoishi maeneo ya vijiji wanawafahamu zaidi Afisa Mtendaji wa kijiji, Afisa Mtendaji wa Kata na Diwani, japokuwa tofauti ni ndogo.¹

Pale ambapo wananchi wameongea na viongozi wao, asilimia kubwa walizungumzia masuala ya kijamii badala ya masuala binafsi ama ya kitaifa. Na mara nyingi, kukutana huko hutokea kwenye mikutano ya umma, majumbani au maofisini mwa viongozi wa ngazi ya kijiji na kata.²

Kielelezo cha 1: Je, unamfahamu, na kama unamfahamu, umewahi kukutana na watu wafuatao?



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa Sauti za Wananchi – Awamu ya 11 (Septemba 2016)

Jambo la 2: Wananchi wachache wanapata taarifa kuhusu masuala ya siasa nchini

Kwa kiwango kikubwa wananchi (61%) wanasema hawapati taarifa kuhusu masuala ya siasa nchini, huku idadi ndogo (4%) wakisema wanapata taarifa za kutosha. Hawa ni wachache kuliko wale wanaosema wanapata taarifa za kutosha kuhusu maendeleo ya sekta za elimu (9%) na afya (9%).³

1 Utafiti wa Sauti za Wananchi – Awamu ya 11 (Septemba 2016)

2 ibid

3 ibid


Kielelezo cha 2: Una taarifa kiasi gani kuhusu masuala ya siasa nchini?



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa Sauti za Wananchi – Awamu ya 11 (Septemba 2016)

Miongoni mwa wale ambao wanapata taarifa za kutosha ama wana taarifa kwa kiasi fulani, sita kati ya kumi (61%) wanapata taarifa kuhusu masuala ya kisiasa kutoka kwenye radio, huku wengine wakipata taarifa hizo kwa kusikia kwa watu (15%), au kwa kupitia kwenye runinga (14%). Vyanzo vingine vimetumika kwa kiwango kidogo sana: 3% pekee wametaja magazeti kama chanzo kikuu cha kupata taarifa kuhusu siasa nchini, huku 1% tu wakitaja mitandao ya kijamii.⁴

Kielelezo cha 3: Je, unapata wapi taarifa kuhusu masuala ya siasa nchini?



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa Sauti za Wananchi – Awamu ya 11 (Septemba 2016)

Jambo la 3: Barabara, maji, afya na elimu ni masuala ambayo wananchi wangependa kuwaaliza viongozi wao waliowachagua

Masuala mengi yaliibuliwa na wananchi walipoambiwa wachague swalii moja ambalo wangependa kuwaaliza viongozi wao waliowachagua. Maji na usafi wa mazingira yalileta mada maarufu yaliyoibua maswali yaliyolekezwa kwa wenyeviti wa vijiji/mitaa.. Barabara, afya na elimu ni mada zilizojitokeza kwenye maswali matano yaliyoulizwa sana kwa wawakilishi wote wanne waliochaguliwa na wananchi.⁵


Kwa Rais Magufuli, swalii kubwa ni suala la mfumuko wa bei, ambalo liliulizwa na wananchi wawili kati ya kumi (18%).⁶

4 ibid

5 ibid

6 ibid

Kielelezo cha 4: Kama ungepata fursa ya kuwaauliza wafuatao swali moja, ungeuliza swali gani? (matokeo ya tano bora ndiyo yaliyooneshwa)



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa Sauti za Wananchi – Awamu ya 11 (Septemba 2016)


Jambo la 4: Vitendo maarufu vya Rais Magufuli ni kuwaondoa wafanyakazi hewa, kutoa elimu ya msingi bure, na kuwasimamisha kazi watendaji wa umma wabadhilifu

Wananchi saba katika kumi wametaja suala la kuwaondoa wafanyakazi hewa kwenye malipo (69%), elimu ya msingi kutolewa bure (67%) na kuwasimamisha watendaji wa umma wanaotuhumiwa kufanya vitendo viovu (61%) kama mambo matatu yanayofanywa na Rais Magufuli ambayo wanakubalina nayo sana.⁷

Baadhi ya mikakati mikubwa ya Rais Magufuli imejitokeza chini kabisa kwenye orodha, likiwemo suala la ukwepaji wa kodi (6%), kupambana na rushwa (1%), kuzuia uagizaji wa sukari (4%), na kupunguza matumizi serikalini yasiyo ya lazima (1%) (hayajaoneshwa kwenye kielelezo).⁸

7 ibid
8 ibid

Kielelezo cha 5: Vitendo vipi vya Rais Magufuli unakubaliana navyo sana?
 (% ya ambao wametaja kila tendo kuwa kati ya matendo matatu bora ya Rais)



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa Sauti za Wananchi – Awamu ya 11 (Septemba 2016)


Jambo la 5: Kitendo cha Rais Magufuli ambacho hakikuungwa mkono na walio wengi ni kuzuia uagizaji wa sukari na kupanga bei elekezi

Walipoulizwa vitendo gani vya Rais Magufuli ambavyo hawakubaliani navyo kabisa, suala kubwa lilitotajwa ni kuzuia uagizaji wa sukari na kupanga bei elekezi. Wananchi watatu kati ya kumi (32%) wanasema hawaafikiani na suala hilo. Idadi ndogo ya wananchi hawakubaliani na usimamishwaji wa watendaji wa umma (9%), kupunguza sherehe za sikukuu za kitaifa na kuzuia shughuli za vyama vya siasa na wabunge (6%).⁹

Hatahivyo, asilimia kubwa ya wananchi (58%) hawakupinga kitendo chochote cha Rais Magufuli.

Vitendo vingi vinavyopingwa na wananchi vimejitokeza chini kabisa kwenye orodha. Hususani, wananchi wachache sana hawakubaliani na uamuzi wa Rais Magufuli wa kusitisha matangazo ya moja kwa moja ya Bunge (3%) au kushindwa kutatua mgogoro wa Zanzibar (0.2%) – haijaoneshwa kwenye chati.

Kielelezo cha 6: Je, ni vitendo gani vya Rais Magufuli ambavyo haukubaliani navyo kabisa?
 (% ya ambao wametaja kila tendo kuwa kati ya matendo matatu mabaya ya Rais)




Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa Sauti za Wananchi – Awamu ya 11 (Septemba 2016)

Jambo la 6: 96% ya watanzania wanaukubali utendaji wa Rais Magufuli tangu alipoingia madarakani, na 68% wanaukubali utendaji wa wabunge wao

Utendaji wa Rais Magufuli tangu alipoingia madarakani umeonekana kujipatia umaarufu mkubwa kwa wananchi, 96% ya wananchi wanasema kuwa "wanakubalina" au "wanakubaliana sana" na utendaji wake.¹⁰

Viwango vya kukubalika kwa makundi mengine ya wawakilishi waliochaguliwa na wananchi navyo viro juu, japokuwa viro chini ya vile vya Rais. Wananchi nane kati ya kumi wanakubaliana na utendaji wa mwenyekiti wao wa kijiji/mtaa (78%) na madiwani wao (74%). Idadi ndogo kidogo (68%) wanakubaliana na utendaji wa wabunge wao.¹¹

Kielelezo cha 7: Ni kwa kiwango gani unakubaliana na utendaji wa watu wafuatao tangu walipoingia madarakani?



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa Sauti za Wananchi – Awamu ya 11 (Septemba 2016)

Tafiti za Afrobarometer zimekuwa zikikusanya takwimu kutoka nchi 34 za kiafrika kuhusu kiwango cha kukubalika kwa marais mbalimbali katika vipindi tofauti. Maswali na mbinu za utafiti wa Afrobarometer unatofautiana kidogo na utafiti wa Sauti za Wananchi, lakini takwimu zinaonesha viwango vya kukubalika vya maraisi wa Tanzania mara nyingi vimekuwa vikiwa karibu kabisa na viwango vya juu vya kukubalika vya marais wote wa Afrika. Mwaka 2005, kuelekea mwishoni mwa kipindi cha pili cha utawala wa Rais Mkapa, kiwango chake cha kukubalika kilikuwa ni 93%, wakati katika vipindi tofauti tofauti marais wa nchi nyingine walifikia viwango vya kukubalika kwa 90% au zaidi. Hii inamhusisha Rais Museveni wa Uganda mwaka 2000 (93%), Rais Kibaki wa Kenya mwaka 2003 (93%), Rais Nujoma wa Namibia mwaka 2003 (90%), Rais Pohamba wa Namibia mwaka 2006 (90%) na Rais Bouteflika wa Algeria mwaka 2013 (90%).¹²

Hata hivyo, kiwango cha kukubalika cha Rais Magufuli katika utafiti mpya wa *Sauti za Wananchi* ni wa kiwango cha juu kuliko viwango vya kukubalika vya marais 128 wa Afrika uliofanywa na Afrobarometer.¹³


10 ibid

11 ibid

12 Afrobarometer: angalia <http://www.afrobarometer.org/online-data-analysis>

13 Utafiti wa Sauti za Wananchi- Awamu ya 11 (Septemba 2016)

Kielelezo cha 8: Viwango vya kukubalika kwa marais, nchi mbalimbali na miaka



(Chanzo: Afrobarometer)

Afrobarometer imekusanya pia takwimu za viwango vya kukubalika kwa wabunge na wananchi wao. Kwa miaka ya nyuma, wabunge nchini Tanzania walifikia viwango vya kukubalika vya kati ya 58% na 67%, juu ya wastani wa viwango vya kukubalika kwa wabunge wa nchi nyininge.¹⁴

Kiwango cha kukubalikwa kwa wabunge wa Tanzania kuititia utafiti huu wa *Sauti za Wananchi* ni 68% unalingana na viwango vilivybainika katika tafiti za awali za Afrobarometer.

Jambo la 7: Wananchi 9 kati ya 10 wanatarajia Rais Magufuli ataendeleza nguvu na kasi yake katika awamu ya kwanza ya uongozi wake

Watanzania walio wengi (88%) wanaamini Rais Magufuli ataendelea na kasi aliyoanza nayo katika uongozi wake mpaka mwisho wa awamu yake ya kwanza. Wananchi 4% pekee hawakubaliana na kauli hii.¹⁵

Kielelezo cha 9: Rais Magufuli ataendeleza kasi yake



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa Sauti za Wananchi – Awamu ya 11 (Septemba 2016)

14

Afrobarometer: angalia <http://www.afrobarometer.org/online-data-analysis>

15


Utafiti wa sauti za Wananchi – Awamu ya 11 (Septemba 2016)

Jambo la 8: Wananchi saba kati ya kumi wanasema ubora wa huduma za umma umeongezeka

Kati ya wale ambao wametumia huduma za umma katika kipindi cha miezi sita iliyopita, saba kati ya kumi wanasema ubora wa huduma umeongezeka. Matokeo haya yanafanana kutoka sekta mbalimbali, kama vile mamlaka za kodi (85%), shule za umma (75%), polisi (74%), mahakama (74%), Vituo vya afya (72%), na mamlaka za maji (67%).¹⁶

Ni vizuri ikaeleweka kuwa hiki si kipimo halisi cha maboresho kwenye utoaji wa huduma za umma, bali ni maoni ya wananchi juu ya ubora wa huduma wanayopata.

Kielelezo cha 10: Kwa maoni yako, je, ubora wa huduma umebadilika katika kipindi cha Rais Magufuli? (Miongoni mwa wale ambao wamepata huduma hizo)




Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa Sauti za Wananchi – Awamu ya 11 (Septemba 2016)

Jambo la 9: Wananchi nane kati ya kumi wanasema watumishi waondolewe pale tu panapopatikana ushahidi wa vitendo viovu

As shown previously, a majority of citizens approve of President Magufuli's dismissal of public officials accused Wananchi wengi wanakubaliana na hatua ya Rais Magufuli ya kuwaondoa watendaji ambao wanatuhumiwa kufanya vitendo viovu. Kwa kuongeza, karibu wananchi (95%) wanasema kuwa watumishi wa umma wanaotoa huduma, kama madaktari na walimu, vilevile maofisa tawala wanawajibika zaidi na kwa ufanisi zaidi. Hatahivyo, wananchi walipotakiwa kufafanua zaidi, walitoa baadhi ya madukuduku yao kuhusu hali ilivyo. Wananchi nane kati ya kumi (76%) wanasema kuwa watendaji waondolewe pale tu ambapo kuna uthibitisho wa vitendo viovu.¹⁷

16 ibid
17 ibid

Kielelezo cha 11: Maoni ya wananchi kuhusu kuwaondoa watendaji wanaotuhumiwa kufanya vitendo viovu




Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa Sauti za Wananchi – Awamu ya 11 (Septemba 2016)

Wananchi tisa kati ya kumi (90%) wanasema kuwa kuwaondoa watendaji wa umma itawasaidia viongozi wengine kutozembea kazi – wakimaanisha kuwa uondoaji wa watendaji wa umma hadharani utakuwa kama mfano kwa wengine.¹⁸

Hata hivyo, karibu nusu ya wananchi (48%) wanakubali kuwa watendaji wa umma watatafuta njia mpya za kuficha maovu yao. Vilevile, wananchi wanne kati ya kumi (37%) wanasema kuwa kuwaondoa watendaji hadharani kutawapunguzia morali ya kazi watendaji wengine.¹⁹

Kielelezo cha 12: kuwaondoa watendaji hadharani...



■ Nakubali/Nakubali sana ■ Sikubali wala sikubaliani ■ Nakataa/Nakataa sana

Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa Sauti za Wananchi – Awamu ya 11 (Septemba 2016)

¹⁸ ibid

¹⁹ ibid

3. Hitimisho

Muhtasari huu umebeba maoni ya wananchi kuhusu utendaji wa serikali ya awamu ya tano, inayoongozwa na Rais Magufuli. Wananchi wana mtazamo chanya kuhusu utendaji wa serikali mpya, huku karibu wananchi wote wakionesha kuukubali utendaji wa Rais mwenyewe. Vitendo vya Rais katika kushughulikia suala la wafanyakazi hewa, kutoa elimu ya msingi bure, na kuwaondoa watendaji wanaotuhumiwa kufanya vitendo viovu – kampeni ya “kutumbua majipu” – vimejizolea umaarufu.

Asilimia kubwa ya wananchi wanasema kuwa watumishi wa umma wamekuwa wasikivu zaidi, wanawajibika zaidi na wanafanya kazi kwa ufanisi zaidi, na hatimaye, ubora wa huduma za umma umeongezeka.

Wananchi wachache wanaonesha kutokuridhishwa na namna Rais Magufuli alivyoshughulikia suala la uchaguzi wa Zanzibar wa mwaka 2015, pamoja na vizuizi alivyoviweka kwa vyama vya siasa na wabunge.

Wananchi wana mashaka kwenye maeneo mawili. Kwanza, katika uondoaji wa watendaji wa umma ambao umejipatia umaarufu mkubwa, wananchi wengi wanasema kuwa watendaji waondolewe mara baada ya kupatikana kwa uthibitisho wa vitendo viovu. Pili, kuzuia uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi na kupanga bei elekezi ya sukari. Maeneo haya mawili yanaonyesha kuwa watanzania hawaungi mkono kila kitu kinachofanywa na Rais. Katika masuala ya kiuchumi pamoja na yale yanayogusa haki za binadamu, muafaka wa waanchi una mipaka na kikomo.

Hatahivyo, kuna viashiria vya mabadiliko makubwa kwenye mitazamo ya wananchi kwa serikali yao. Miaka iliyopita, baada ya uzoefu wa muda mrefu, wananchi walikuwa na matarajio hafifu ya ubora wa utendaji wa serikali. Jambo hili lilishusha matarajio ya wananchi, likawakatisha tamaa na kuuruhusu utendaji mbovu kuendelea bila kuhojiwa na mtu yeoyote. Kwa mfano, mwaka 2014, zaidi ya nusu ya wananchi walisema kuwa suala la rushwa haliwezi kutatuliwa,²⁰ na robo tatu walisema nchi ilikuwa ikielekea pabaya.²¹ Lakini muhtasari huu unaonesha kuwa wananchi wana matarajio makubwa kuwa serikali ya awamu ya tanoinaweza kubadilisha hali ya mambo.

Matarajio makubwa sana yana changamoto mbili kuu. Yakiwa makubwa mno, yakazidi uwezo wa serikali kuyatimia, wananchi wanaweza kukata tamaa tena na kurejea, kimtazamo, kule walipotoka. Aidha, yanaweza kuchochea maamuzi ya serikali yatakayobana utawala wa sheria, au yatakaodhoofisha demokrasia hii change, au kuuathiri ustawi wa uchumi.

Lakini, yakinolewa vizuri na kufanyiwa kazi na uongozi wa umma, matarajio makubwa yanaweza kujenga utamaduni mpya wa wananchi kufuatilia utendaji, kuhoji maamuzi, na kutegemea viwango bora zaidi vya utendaji na matokeo yake kutoka kwa serikali yao.

20 Utafiti wa Sauti za Wananchi, Juni 2014
21 Afrobarometer 2014